# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

## GREDI 5 - 2025

Wings 005

## KISWAHILI : INSHA

**Muda: Dakika 40**

**(Alama 10)**

**Andika insha ya kusisimua inayoanzia kwa maneno haya:**

**Siku ya Jumamosi ilikuwa siku ya kawaida kama nyingine. Niliamka asubuhi.........................................**



for more exam 0703752217

CamScanner

CamScanner

# TARGETER WINGS
## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI
## GREDI 5 - 2025
# SHUGHULI ZA KISWAHILI

Wings 005

Muda: Saa 1

***KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA***

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali**

**Mwalimu A** : Shikamoo Mwalimu Jane! Umeamkaje leo?

**Mwalimu B** : Marahaba Mwalimu John. Nimeamka salama kabisa, asante. Na wewe je?

**Mwalimu A** : Salamu tu. Nilitaka kujua kama utakuwepo kwenye kikao cha jioni leo.

**Mwalimu B** : Ndio, nitakuwepo. Kuna jambo maalum litakalojadiliwa

**Mwalimu A** : Ndiyo, tunatarajia kupanga ratiba mpya ya mitihani na pia kuzungumzia maendeleo ya wanafunzi wa gredi ya tano

**Mwalimu B** : Ah. Sawa kabisa. Ni[illegible] imeandaa takwimu zote kabla ya kikao.

**Mwalimu A** : Vizuri sana . T[illegible] baadaye.

**Mwalimu B** : Sawa asante. Tutaonana.

1. Ni walimu gani wana[illegible] katika mazungumzo haya?
   A. John na Jane
   B. John na Joy
   C. Jane na Joy
   D. Yona na Yuda
2. Mazungumzo haya yan[illegible] wakati gani wa siku?
   A. Usiku
   B. [illegible]
   C. Asubuhi
   D. [illegible]
3. Kikao kilichotajwa kitafanyika lini?
   A. Siku iliyofuata asubuhi
   B. Siku hiyo jioni
   C. Siku iliyofuata jioni
   D. Siku hiyo asubuhi
4. Mwalimu Jane angefanya nini kabla ya kikao?
   A. Kuunda ratiba
   B. Kuleta matokeo ya gredi ya tano
   C. Kuongea na wanafunzi wa gredi ya tano
   D. Angeandaa takwimu
5. Ni da[illegible] ambayo maendeleo ya wanafunzi wake yangejadiliwa?
   A. Gredi ya nne
   B. Gredi ya tano
   C. Gredi ya sita
   D. Gredi ya tisa

Call for more exam 0703752217



CamScanner

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi 9**

Katika Kijiji kidogo kilichozungukwa na milima, aliishi mvulana aliyeitwa Juma. Kila siku, Juma alikuwa akitembea kwa umbali kwenda mtoni kuchota maji kwa ajili ya familia yake . Alikuwa na vibuyu viwili, kimoja kipya na kingine kilichokuwa na ufa mdogo. Kila aliporudi nyumbani, kibuyu kipya kilijaa maji lakini kile chenye ufa kilikuwa kimepoteza nusu ya maji. Hii ilimhuzunisha sana Juma, lakini hakuwa na lingine la kufanya.

Siku moja kibuyu kilichokuwa na ufa kikamwambia Juma, "samahani kwa kukusumbua kila siku, sipaswi hata kuwa hapa." Juma akatabasamu na kusema, " je, umeona maua yanayochanua upande wako wa njia?" kibuyu kikashangaa.

Juma akaendelea , "kila siku, maji yanayotoka kupitia ufa wako yamekuwa yakimwagilia maua hayo. Sasa Kijiji chetu kina maua ya kupendeza kwa sababu yako." Kibuyu kikanyamaza, kikiwa kimejawa na furaha. Kilijua kuwa, hata kwa udhaifu wake, kilikuwa cha thamana.

6. Juma alikuwa anaishi wapi?
   - A. Mjini karibu na Soko
   - B. Kijiji kilichozungukwa na milima
   - C. Katika ufuko wa Bahari na milima
   - D. Jangwa la Sahara
7. Juma alikuwa anatumia vibuyu vingapi kuchota maji?
   - A. Kimoja
   - B. Viwili
   - C. Vitatu
   - D. Vinne
8. Kibuyu kimoja kilikuwa na shida gani?
   - A. Kilikuwa Kizito sana
   - B. Kilikuwa kidogo mno
   - C. Kilikuwa na ufa mdogo
   - D. Kilikuwa cha plastiki
9. Ujumbe mkuu wa hadithi hii ni upi?
   - A. Tunapaswa kuwa wakali kwa vitu vilivyovunjika
   - B. Lazima vitu vyote viwe vipya ili vitumike
   - C. Kila mmoja wetu ana dhamana hata katika mapungufu yake
   - D. Maji ni muhimu kwa maisha

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 10 hadi 12**

Sungura alikuwa mwepesi na mwenye majivuno. Alimcheka Kobe kwa upolepole wake. siku moja katika matembezi yao, Sungura alimtania Kobe kwa kusema " pole sana rafiki yangu, unatembea polepole kama mzigo! Kobe akamjibu kwa utulivu, " twende mbio, tuone nani atashinda."

Mbio zikaanza. Sungura alikimbia kwa kasi, lakini akasema, " nitalala kidogo, bado nitamshinda Kobe." Alilala usingizi mzito. Kobe, bila kusimama, aliendelea kutambaa. Alipomfikia Sungura, hakusema chochote alimpita na kuendelea na mbio. Alipofika mwisho wa mbio alishangiliwa na Wanyama wote. Sungura alipoamka, alipata kuwa tayari alikuwa ameshindwa.

10. Sungura alimwambia nini kobe mwanzoni?
    - A. " twende tukale."
    - B. " wewe ni mwepesi sana."
    - C. " pole sana, unatembea kama mzigo."
    - D. " wewe ni mwenye majivuno "



CS CamScanner

11. Kwa nini sungura hakushinda mbio?
A. Alianguka njiani
B. Aliumia mguu
C. Alilala njiani kwa kujiamini
D. Alikuwa na njaa

12. Kobe aliendelea vipi katika mbio?
A. Kwa kukimbia haraka
B. Kwa kuruka
C. Kwa kutambaa bila kusimama
D. Kwa msaada wa ndege

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 13 hadi 15**

Wanyama wa pori walikumbwa na ukame mkubwa. Maji yalikuwa yamekauka kila mahali. Wote walihangaika sana – Tembo, Pundamilia na hata Simba walikuwa na kiu, lakini kulikuwa na kisima kimoja tu kilichokuwa na maji, ila kilikuwa kirefu mno. Hakuna mnyama aliyeweza kufikia maji hayo. Wote walijaribu, lakini walishindwa.

Nyani akafikiri na kusema, " Sote tunapaswa tulete mawe madogo na kuyaweka ndani ya kisima." Wanyama walicheka , lakini wakajaribu wazo la nyani. Walileta mawe na kuyaweka ndani ya kisima moja baada ya nyingine. Kadri mawe yalivyozidi, maji yakaanza kupanda juu. Hatimaye, maji yalifika juu kabisa na kila mnyama aliweza kuyanywa .

13. Ni tatizo gani lililowakumba Wanyama ?
A. Mvua nyingi zilizosababisha mafuriko
B. Ukame uliosababisha ukosefu wa maji
C. Kulikuwa na Wanyama wengi porini
D. Kulikuwa na ugomvi kati ya Simba na Tembo.

14. Kisima cha maji kilikuwa na shida gani?
A. Kilikuwa kimejaa mchanga
B. Kilikuwa kimevunjika
C. Kilikuwa kirefu sana kufikia maji
D. Kilikuwa na mawe ndani

15. Ni nani aliyetatua tatizo la kufikia maji kisimani?
A. Pundamilia
B. Tembo
C. Simba
D. Nyani

## SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu nafasi zilizoachwa.***

Kenya ni nchi yenye mbuga nyingi za Wanyama. Mbuga maarufu zaidi hapa nchini Kenya ni __16__. Wanyama wanaopatikana kwenye mbuga hiyo ni Pamoja na simba, tembo na __17__.Watu wa jamii ya__18__ huishi karibu na mbuga hiyo. Jamii hiyo huvaa __19__ na wao hupenda kula chakula kama vile __20__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 16. | Serengeti | Tsavo | Mikumi | Ngorongoro |
| 17. | farasi | nyati | ngamia | kondoo |
| 18. | Waswahili | Wameru | Wamasai | Wagikuyu |
| 19. | kizibao | kaptura | surupwenye | mavazi ya kijadi |
| 20. | wali wa nazi | ugali wa maziwa | asali | samosa |



CamScanner

## MATUMIZI YA LUGHA

***Jibu maswali yafuatayo kulingana na maagizo uliyopewa.***

**21. Chagua nomino dhahania katika sentensi hii:**

"Upendo ni jambo la maana katika maisha"

A. upendo B. jambo

C. maana D. maisha

22. Ni lipi kati ya maneno yafuatayo lina viambishi vya wakati uliopita?

A. Anaimba B. Ataimba

C. Aliimba D. Huimba

**23. Chagua jibu sahihi**

Mama alienda sokoni ___________ kununua matunda.

A. kwa sababu B. ili

C. kama D. lakini

24. Neno lipi ni kinyume cha 'baridi'?

A. Barafu B. Maji

C. Joto D. Kali

**25. Chagua sentensi sahihi:**

A. Baba alipika chakula kitamu sana.

B. Baba chakula kitamu sana alipika.

C. Kitamu sana baba alipika chakula

D. Alipika kitamu sana baba chakula.

26. Katika sentensi: '**mtoto alikula chakula chake vizuri**' neno "**vizuri**" **ni nini?**

A. Kitenzi B. Kielezi

C. Kivumishi D. Kiunganishi

27. Ni lipi kati ya maneno haya ni neno la heshima?

A. Kuja B. Samahani

C. Kimbia D. Enda

**28. Kamilisha methali:-**

Mtoto umleavyo ndivyo_______________.

A. akuwapo B. atakuwa

C. anakuwa D. akuavyo

**29. Chagua ukanusho sahihi wa sentensi ifuatayo:**

Aliandika barua

A. Aliandika barua si B. Hakuandika barua

C. Haliandika barua D. Hajaandika barua

**30. Wingi wa sentensi ifuatayo ni**

Mti mrefu unaonekana

A. Miti mirefu inaonekana B. Mti mrefu unaonekana

C. Miiti refu inaonekana D. Miti ndefu inaonekana.



CamScanner